



## EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

# TANGAZO LA ZABUNI YA KUTOA HUDUMA ZA USHAURI WA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII KWENYE MRADI WA BOMBA LA MAFUTA LA AFRIKA MASHARIKI NCHINI UGANDA - NAMBA YA KUMBUKUMBU: 0010004926

Total east Africa Midstream B.V (TEAM) inawakaribisha makandarasi wenye uzoefu na sifa ambao wameonyesha uwezo, nia na ambao wako tayari kutoa huduma za ushauri wa athari za kimazingira na kijamii kwenye mradi wa bomba la mafuta la Afrika Mashariki (EACOP) nchini Uganda, kutuma maombi yao kwenye zabuni hii. Mradi wa EACOP unajumuisha bomba la mafuta lililofukiwa chini ya ardhi nchini Tanzania na Uganda likiwa na mfumo wa umeme wa kuleta joto pamoja na miundombinu iliyo juu ya ardhi na kituo cha kuhifadhiha mafuta cha baharini na miundombinu ya kusafirishia mafuta nje ya nchi karibu na Tanga. Maendeleo ya mradi yanajumuisha uhandisi maombi ya kisheria na idhini, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya miundombinu hii.

### Maelezo mafupi kuhusu huduma

Mahitaji ya huduma za ushauri wa kimazingira na kijamii kwa ajili ya mradi wa EACOP yanajumuisha taratibu za hali ya juu za kiusalama na uelewa mkubwa kuhusu mazingira na kufanya tafiti za kimazingira ikiwa ni pamoja na tathmini za athari za kimazingira, maandalizi ya mipango ya kimazingira na kijamii na ukaguzi wa kimazingira na kijamii, ushirikishaji wa wadau,

vikao vya kutoa taarifa, kurekodi malalamiko na kuwasilisha maombi ya ya kibali

### Sifa za msingi:

- Usajili kwenye kanzi data ya watoa huduma iliyopo kwenye Mamlaka ya Petroli ya Uganda kwa ajili ya watoa huduma kwenye sekta ya mafuta na gesi
- Uzoefu kwenye kufanya tathmini za athari za kimazingira na kijamii kwenye miradi mikubwa na midogo hususani kwenye sekta ya uchimbaji madini
- Uzoefu wa kufanya tafiti za kimazingira na kijamii
- Uzoefu wa kufanya ukaguzi wa kimazingira na kijamii kwenye miradi mikubwa kwa ajili ya mahitaji ya kisheria au kwa ajili ya ufadhili wa taasisi za kimataifa
- Uzoefu wa kuwashirikisha wadau na kutoa taarifa kwenye miradi mikubwa
- Upatikanaji mzuri wa rasilimali ikiwa ni pamoja na vifaa, mifumo na wafanyakazi wenye sifa
- Uwezo wa kifedha kwa ajili ya kutekeleza kandarasi husika
- Sera inayofaa ya afya, usalama, mazingira, jamii na ubora
- Dhamira ya kutumia bidhaa za ndani

Makampuni yanayotaka kutuma maombi inabidi yawe na sifa za msingi na yawe na uwezo wa kutoa huduma zilizotajwa hapo juu, yaombe fomu ya zabuni kwa kutuma barua pepe kwa: [ep.prequalification-ugep@total.com](mailto:ep.prequalification-ugep@total.com) kabla ya tarehe **6 Februari 2018, saa 11.00 jioni kwa saa za Kampala.**

**Masahishio :** Barua pepe kuhusu wito wa zabuni ya kutoa huduma za ushauri wa athari za kimazingira na kijamii kwa ajili ya mradi wa bomba la mafuta la Afrika Mashariki lililochapishwa Alhamis, tarehe **11 Januari 2018 imebadilishwa.** Makampuni yaliyotuma maombi kwenye barua pepe hiyo yanatakiwa kutuma tena maombi kwa barua pepe iliyoonyeshwa hapo juu.